OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

Simu Na. 027-2530022
Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz
Tovuti:www.hanangdc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Hanang,
2 Barabara ya Amani,
S.L.P. 2,
27382 Ganana – Hanang,
MANYARA.

# TANGAZO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' anawatangazia Wananchi wote fursa ya ufunguaji/usafishaji wa mashamba pori ndani ya shamba la Bassotu plantation ambapo msafishaji ataruhusiwa kulitumia eneo alilosafisha kwa misimu miwili (2) kwa gharama nafuu ya **Tsh. 30,000/=** kwa ekari kabla ya kulikabidhi kwa Halmashauri au kuanza kulilipia kwa utaratibu wa kawaida kuanzia msimu wa tatu.

Kwa yeyote mwenye uhitaji wa kufanya kazi hii, atalazimika kuwasilisha barua ya maombi Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ikiwa imepitishwa kwa **Afisa Mtendaji wa Kata ya Mulbadaw**, kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha katika kufanya kazi hii, mashariti yafuatayo yatazingatiwa:-

1. Miti na uoto mwingine kwenye kingo za shamba (Contours) pamoja na maeneo yenye makorongo haitakatwa wala kuharibiwa, itabaki kwa ajili ya kukinga mmomonyoko wa udongo.

2. Usafishaji wa shamba utahusisha kuondoa vichaka/miti na kuchimba visiki na kuviondoa shambani.

3. Endapo msafishaji atatumia miti aliyoikata kuchoma mkaa (**kwa kuzingatia taratibu za uchomaji mkaa**) atachukua nusu (50%) ya mauzo ya mkaa utakaopatikana na nusu (50%) inayobaki itawasilishwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri.



CamScanner

4. Msafishaji **HATARUHUSIWA** kupanda mazao ya muda mrefu, bali mazao ya msimu mmoja mmoja.

5. Mwombaji atakayekubaliwa ataingia mkataba rasmi wa maandishi na Halmashauri baada ya uhakiki wa eneo atakalolisafisha kufanyika.

Kwa maelezo zaidi; wasiliana kwa namba 0688 368 258 au 0784 725 922.

PP

*Teresia A. Irafay*
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA
HANANG

04/09/2025